TANGAZO LA SERIKALI NA. 215 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 511 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni 6 kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(1) Halmashauri itahakikishwa kwamba ada au ushuru unakusanywa wakati wote katika maeneo yake.";

(b) kufuta kanuni ndogo ya (2); na

(c) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo za (3) na (4) kuwa kanuni ndogo za (2) na (3) mtawalia.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Sehemu ya Nane ya Jedwali la Kwanza kwa kufuta kipengele cha 5 na kukiandika upya kama ifuatavyo:

"5. Tani 13 na kuendelea 25,000/=".

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*